

**Ujumbe kutoka kwa Bi Audrey Azoulay, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO,
Kwa Kongamano la
103 la Ulimwengu la Chama Cha Esperanto Ulimwenguni.
Lisbon, Julai 29, 2018**

Ninafurahia kutuma maneno haya ya msaada kwa washiriki wa Kongamano la 103 la Ulimwengu la Chama Cha Esperanto ulimwenguni.

Mna bahati ya kukutana katika jiji hili zuri la Lisbon, jiji linalohusishwa na historia kubwa ambayo imejengwa kwenye makutano ya barabara na tamaduni mbalimbali, jiji lililowazi kwa ulimwengu, magharibi mwa peninsula ya Iberia.

Sina shaka kuwa mfumo huu bora utafanikiwa kuhimiza ushirikiano wenye manufaa kwenu.

Kama unavyojua, UNESCO inaunga mkono mafundisho ya Kiesperanto kwa miaka mingi.

Ni kweli kwamba Shirika letu linashirikiana na harakati za kiesperanto kwa manufaa ya pamoja: matumaini katika kujenga ulimwengu wa amani, umoja thabiti kati ya watu, heshima katika tofauti za utamaduni, mshikamano uvukao mipaka.

Kiini cha maadili haya yote ni uwezo wa kuongea, kusikiliza na kuwasiliana.

Lugha, muelekeo wa majadiliano haya, hufanya chombo muhimu ili kufikia malengo ambayo tunapaswa kutambua, na pia kwa ulinzi wa maadili yetu.

Tunapaswa kuzilinda lugha, hasa lugha za nadra, lugha za asili, ambazo tunajua kuwa sasa zinapotea kwa kiwango cha lugha moja baada ya wiki mbili - ambayo ni kupoteza kwa uhakika kwa urithi wa binadamu.

Tunapaswa pia kutetea lugha mbalimbali, sio tu kwa sera za umma, bali pia katika nafasi ya mtandao, kwa kuzipatia lugha tofauti tofauti na tamaduni pia katika jamii nafasi ya kuishi. Ili kila mtu aweze kujifunza kuhusu historia yake, utambulisho wake, kutoka kwa vyanzo vya mfano vya kikundi chake cha asili.

Jitihada hizi pia ni zakwako.

Kwa sababu Kiesperanto hakitaki kufuta wingi wa lugha zinazozungumzwa ulimwenguni; Kwa upande mwingine, kinawakilisha chombo kifaacho cha mazungumzo kwa kuzingatia lugha zote, iwe wachache au wengi, na kutambua kuwepo kwa kundi la wasemaji, bila kutegemea hegemoni yoyote ya kiuchumi, kisiasa au kiutamaduni.

Kuzungumza Kiesperanto ni kwenda kwenye mfumo wa ushauri wa ulimwengu, kuwa raia wa ulimwengu - bila kuacha viungo vyake tofauti.

Mada iliyochaguliwa kwa mkutano wenu mwaka huu ni: "Mila, lugha, utandawazi: tunaelekea wapi sasa?"

Mwelekeo teule hakika ni ule ambao, harakati zenu na Shirika letu vimeonyesha kwa miaka mingi: kushiriki zaidi na zaidi katika kuokoa na kusaidia sehemu hii muhimu ya urithi wa kibinadamu usio vitu, ambao ni lugha; kulinda utofauti wa lugha na kuhimiza elimu ya lugha mbalimbali.

Hivyo tutafanikiwa katika kujenga ulimwengu ulio wazi zaidi, wenye umoja na amani.

"Sauti nyingi, ulimwengu mmoja"- hii ni kauli mbiu ya chombo chetu maarufu cha *Mjumbe was UNESCO*.

"Multaj voĉoj, unu mondo" ndivyo ile dhana tunayoshiriki inavyo tafsiriwa kwa Kiesperanto - na ambacho kimeandikwa kwenye toleo la gazeti letu, ambalo limejitokeza tangu hivi karibuni katika Kiesperanto: *Unesko-Kuriero*.

Hatimaye ninapenda kuwasilisha kwa niaba ya UNESCO, na kuwatakia kila la kheri na mafanikio katika kongamano lenu.

Audrey Azoulay,
Mkrugenzi Mkuu wa UNESCO

- - -

*El Esperanto en la Svahilan lingvon tradukis John E. Magessa, Tanzanio
Kutoka Kiesperanto kwenda Kiswahili, imetafsiriwa na John E. Magessa, Tanzania*

Message de Audrey AZOULAY, Directrice générale de l'UNESCO, à l'occasion du Congrès mondial de l'association universelle d'Esperanto, Lisbonne, 29 juillet 2018:

<http://www.linguistic-rights.org/unesco/2018-29-07-LISBONNE-Congres-esperanto-Vfinal-AZOULAY.pdf>